*Mulika, Na. 44 (1), 14-35*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# "Korona wewe ni nani?" Uchambuzi Kilongo wa Ushairi kama Mkakati wa Kupambana na UVIKO-19

*Angelus Mnenuka*[1]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t1.2

**Ikisiri**

Miongoni mwa matukio makubwa yaliyoikumba dunia kuanzia mwaka 2020 ni mlipuko wa maradhi ya UVIKO-19. Kazi mbalimbali za sanaa zilitumiwa katika kuhamasisha kampeni ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu uliozua hofu kubwa duniani. Kwa kuwa kazi za sanaa huakisi ridhimu ya mawazo ya jamii, na kwamba wasanii ni zao la jamii, nyimbo nyingi za kuhamasisha vita dhidi ya UVIKO-19 zilisheheni mawazo yaliyotia hofu zaidi. Kinyume na matarajio ya wengi, Mrisho Mpoto alitumia mtindo tofauti. Badala ya kuendelea kuitia hofu jamii ili ifuate taratibu za kujikinga kama walivyofanya wengine, yeye aliitia jamii ujasiri na kuhamasisha kuondoa woga katika mapambano dhidi ya UVIKO-19. Katika makala haya, wimbo mmoja umeteuliwa kati ya nyimbo 25 kutokana na upekee wa mtindo uliotumiwa kuwasilisha maudhui yenye kuhamasisha mapambano dhidi ya UVIKO-19. Makala haya yametumia mkabala wa elimumitindo kuchambua mtindo wa wimbo wa "Kwaheri Corona" kwa kutumia Nadharia ya Uchambuzi Kilongo kama ilivyoasisiwa na Norman Fairclough. Matokeo yanaonesha kuwa msanii alitumia mtindo wa majigambo na ushairi wa kivita kama mbinu ya kujenga ujasiri kwa kukidunisha kirusi cha Korona na kuikweza jamii ya Watanzania. Mtindo huo ulilenga kuondoa woga uliotanda katika jamii nzima wakati wa mapambano dhidi ya janga la UVIKO-19.

## 1.0 Utangulizi

Matukio makubwa katika jamii kama vile vita, mafuriko, ukame, baa la njaa au mlipuko wa maradhi huacha simulizi zinazokumbukwa. Mara nyingi, simulizi hizo hufumbatwa pia katika kazi za sanaa, hususani fasihi simulizi. Ushairi, simulizi na semi mbalimbali hufumbata baadhi ya matukio hayo kwa sababu baadhi ya vipengele vya tanzu hizo hutokana na matukio hayo (taz. Bryant, 2005; Gunderson, 2010; Kipacha, 2015). Miongoni mwa matukio makubwa yaliyoikumba dunia mwaka 2020 ni mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya Korona – UVIKO-19. Ugonjwa huu ulianzia katika mji wa Wuhan ulioko katika Jimbo la Hubei nchini China na baadaye kuenea maeneo mbalimbali duniani (Tarimo na Wu, 2020; Hamisi, Dai na Ibrahim, 2023). Kama ilivyo ada kwa wasanii, kazi za kisanaa zilitungwa katika maeneo tofautitofauti barani Afrika kwa malengo tofauti kama vile kuhamasisha umoja katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo,

[1] Profesa Mshiriki, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Baruapepe: amnenuka@gmail.com / amnenuka@udsm.ac.tz

kuwafariji waliopoteza ndugu na jamaa, na kuwaombea marehemu (taz. Thompson, Nutor na Johnson, 2021; Otieno, 2021; Habib, 2022; Ndiaye na Rowley, 2022). Nchini Tanzania pia, nyimbo mbalimbali ziliimbwa ili kuhamasisha watu kujikinga dhidi ya maradhi hayo. Mbali na sanaa ya vibonzo na ufutuhi wa hapa na pale (taz. Mnenuka, 2024), ushairi pia ulitumiwa kama nyenzo mojawapo ya kampeni dhidi ya maradhi ya UVIKO-19. Miongoni mwa nyimbo hizo ni "Kwaheri Corona" ulioghanwa na Mrisho Mpoto, msanii maarufu wa kughani mashairi ya Kiswahili na mwigizaji anayetokea nchini Tanzania. Wimbo huu, tofauti na nyimbo zingine, umetumia mtindo wa kipekee ambapo msanii anazungumza na kirusi cha Korona huku akikitisha kuwa hakitaweza kuidhuru Tanzania. Makala haya yamechambua upekee wa mtindo uliotumiwa na namna ulivyofikisha maudhui. Kwa kuwa upekee wa wimbo huu umetokana na mtindo uliotumiwa, sehemu inayofuata inafafanua kwa muhtasari kuhusu dhana ya mtindo.

## 1.2 Dhana ya Mtindo

Mtindo ni dhana changamani na inatumiwa kwa namna tofautitofauti kulingana na mrengo wa mtumiaji; matokeo yake hakuna fasili moja inayofumbata dhana zote pamoja (Hendricks, 1980; Kahigi, 1997; Čarkič, 1996; Leech na Short, 2013; Herrmann, Van Dalen-Oskam na Schöch, 2015). Pamoja na uchangamani huo, Leech na Short (2013) wanasisitiza kuwa maana ya kawaida ya mtindo haina utata. Dhana ya mtindo, wanazuoni hawa wanaendelea kufafanua kuwa, inaingia katika utelezi mkubwa pale inapotumiwa na wanazuoni kama dhana ya kiuchambuzi. Pamoja na fasili za mtindo kutofautiana, dhana za mtindo zinaweza kuwekwa katika makundi makubwa mawili, yaani mtindo kama uteuzi na mtindo kama utofauti (taz. Rosengren, 1972; Walpole, 1980; Kahigi, 1997). Kwa mujibu wa wanazuoni hawa, mtindo kama uteuzi unaweza kuelezwa kama uamuzi wa msanii kutumia ala mbalimbali za kisanaa miongoni mwa ala nyingi zilizomo katika gimba la msanii. Kwa upande mwingine, mtindo kama utofauti unaweza kuelezwa kama uamuzi wa msanii kutumia mitindo inayokiuka kaida za utanzu fulani katika kipindi fulani. Rosengren (1972) anasisitiza kuwa aina hii ya mtindo inaweza kubainika bila kulinganisha na matini zingine kwa sababu ukiukaji wa kaida upo bayana. Hata hivyo, Kahigi (1997) anahitimisha kwa kudai kuwa dhana hizo hazina tofauti ya msingi kwa sababu upande mmoja unachunguza uundaji wa matini na upande mwingine unachunguza matini iliyokamilika.

Baada ya kufanya mapitio ya kina ya matapo na mikondo sita ya fasili za mtindo tangu karne ya 18, Herrmann, Van Dalen-Oskam na Schöch (2015) wanafasili mtindo kama sifa ya matini inayoundwa na mseto wa nduni rasmi zinazoweza kubainishwa kitakwimu au kitaamuli. Maana yake, mtindo unajumuisha nduni mbalimbali zinazofumbatwa katika matini ya aina yoyote kwa namna mbalimbali. Hata hivyo, pamoja na mseto huo wa nduni kufinyangwa kiuchangamani, nduni hizo zinaweza kubainishwa kitakwimu na kitaamuli. Kwa ujumla, dhana ya

mtindo kwa mtazamo wa Kahigi (1997) na Herrmann na wenzake (2015) ni upekee wa vipashio vinavyounda matini. Uchambuzi wa wanazuoni hawa umekitwa zaidi katika upekee wa vipashio kuliko namna mtindo unavyoathiri maudhui ya matini.

Dhana ya mtindo inafafanuliwa pia na Miloslav Čarkič ambapo baada ya kutalii ufafanuzi wa mtindo kutoka kwa wanazuoni mbalimbali tangu enzi za Plato na Aristotle, anaeleza kuwa mtindo ni upekee ambao haujirudii katika lugha na aina yoyote ya ujielezaji (Čarkič, 1996: 334). Maana yake, hata msanii hawezi kurudia mtindo uleule katika kazi zake mbalimbali kwa sababu muktadha wa utunzi unaathiriwa na masuala ya kiakili, kihisia, kiimani na kikazi. Aidha, muktadha wenyewe hauwezi kujirudia kwa namna ileile. Kifupi, anaeleza kuwa mtindo ni upekee na upekee hujitokeza katika tukio au kazi moja tu.[2] Čarkič (1996) anasisitiza kuwa katika sanaa na tasnia nyingi, dhana ya mtindo inaendana na ubunifu, yaani msanii anatakiwa kuwa mbunifu ili alete mtindo mpya. Anahitimisha kwa kueleza kuwa mtindo unajumuisha umbo la nje (fani) na maudhui ya ndani (muundo). Kwa hiyo, mtindo unajumuisha fani na maudhui pamoja. Ujumuishaji wa umbo la nje na umbo la ndani unaonesha kuwa mtindo si urembo tu wa maudhui bali ni sehemu muhimu ya maudhui ya matini.

Kwa ujumla, fasili mbalimbali za mtindo zimegawanyika katika mitazamo miwili: mosi, mtazamo wa *uwili*. Mtazamo huu unatenganisha maudhui na mtindo kama dhana mbili zinazojitegemea. Pia, kwa upande mwingine, ni mtazamo wa *umwe*, yaani mtindo na maudhui havitenganishiki (taz. Leech na Short, 2013; Tyler, 2021). Kwa kuwa mtindo huukiliwa na maudhui katika uundaji wa matini na katika uchambuzi, makala haya yanaafiki na kutumia dhana ya mtindo ya umwe kwa sababu mtindo huhusika katika pande zote mbili, yaani katika uundaji wa matini ambapo msanii huteua ala zilizopo na kuleta upya wa kazi yake; halikadhalika, kwa upande wa uchambuzi wa matini ambapo mhakiki hutumia mbinu na nadharia zinazoakisi mtindo wa uandishi wa matini. Kwa hiyo, mtindo uliotumiwa na Mrisho Mpoto haupaswi kuchukuliwa kama kipengele cha ziada bali ni sehemu muhimu ya maudhui ya matini na uchambuzi wake unapaswa kuzingatia upekee wa vipashio vya wimbo huo ili kuelewa barabara maudhui na mantiki ya mtindo huo.

Makala haya yamepangiliwa kama ifuatavyo: Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambao unatoa mawazo ya jumla ya makala kuhusu fasihi simulizi na matukio katika jamii, hususani mlipuko wa maradhi ya UVIKO-19 ulivyochangia kuibuka kwa nyimbo na mitindo mbalimbali kama ule wa Mrisho Mpoto. Sehemu ya pili ni maelezo kuhusu methodolojia ambayo inachambua namna utafiti huu

[2] Hoja hiyo inapingana na ile ya Tyler (2021) anayedai kuwa mtindo wa mwandishi unaweza kutumiwa katika kazi zake kadhaa.

ulivyofanyika. Baada ya methodolojia, sehemu inayofuata ni nadharia, yaani, Nadharia ya Uchambuzi Kilongo kwa kutumia mkabala wa Norman Fairclough na sababu za kutumia nadharia hiyo. Sehemu ya tatu inahusu uchambuzi wa matini katika ngazi zote tatu kwa mujibu wa Fairclough (1992a) ambazo ni uchambuzi wa matini, utendaji wa matini na muktadha wa kijamii; na hatimaye hitimisho. Sehemu inayofuata inafafanua methodolojia ya makala haya.

## 2.0 Methodolojia

Makala haya yametumia mkabala wa kitaamuli. Data zilikusanywa kupitia vyombo vya habari kwa kuusikiliza wimbo teule na matangazo yanayoambatana na ujumbe wa wimbo huo. Hata hivyo, usikilizaji makini ulifanyika baada ya kuupakua wimbo huu katika mtandao wa *YouTube* ambapo ulinukuliwa na kutoa nafasi ya kuchambua matini andishi kwa uangalifu zaidi. Data zilichambuliwa kwa ngazi tatu kwa mujibu wa Nadharia ya Uchambuzi Kilongo. Katika ngazi ya awali, vijenzi vya matini vilichambuliwa ambapo miundo midogomidogo kama vile vipashio mbalimbali vya sentensi vilichambuliwa. Kisha katika ngazi ya pili, utendaji wa matini umefafanuliwa ambapo imebainishwa kuwa matini hii ni wimbo uliorekodiwa na kupigwa katika vyombo vya habari na kusambaa katika mitandaopepe ya kijamii ili jamii ipate ujumbe. Hatimaye, katika muktadha wa kijamii matini imechambuliwa kwa kuzingatia mazingira ya wakati huo wa mlipuko wa UVIKO-19. Mifano michache imetumiwa ili kusisitiza hoja zilizotolewa. Matini zimechambuliwa kwa kufuata misingi ya kinadharia kama inavyofafanuliwa katika sehemu inayofuata.

## 3.0 Nadharia

Data za makala haya zimechambuliwa na kufasiriwa kwa kutumia Nadharia ya Uchambuzi Kilongo kwa mkabala wa Norman Fairclough (1992a). Nadharia hii imesaidia kubaini vipashio vya matini teule, utendaji wake na muktadha wake kijamii ulivyoweza kutumiwa kutoa hamasa katika mapambano dhidi ya UVIKO-19. Nadharia hii imetumiwa kwa sababu inasaidia kubaini mtindo uliotumika katika muktadha wa kijamii pamoja na maudhui ya matini, hususani wakati ulipotungwa na kutumbuizwa.

Uchambuzi kilongo ni dhana pana inayotumiwa katika taaluma nyingi kama vile sosholojia, filosofia, historia, fasihi, utamaduni, anthropolojia, saikolojia na isimu (Mills, 2004; Wodak, 2006). Ili kuelewa dhana ya uchambuzi kilongo, ni muhimu kutoa ufafanuzi mfupi kuhusu dhana ya kilongo.

### 3.1 Kilongo

Kilongo ni miongoni mwa dhana tepetevu na telezi kwa sababu haiwasilishi wazo moja na inafumbata mitazamo mingi (Thornbury, 2010; Wodak, 2011). Utelezi huu unatokana na dhana hii kutumiwa katika nyuga nyingi. Kwa kuwa kila mchambuzi hutoa fasili inayoendana na uga wake, hakuna fasili moja

inayofumbata maana zote. Huku baadhi ya wanazuoni wakiifafanua dhana hii kwa mtazamo finyu kama maana ya matini simulizi au andishi inayopatikana nje ya mipaka ya sentensi (Guardado, 2018), wataalamu wengine wameifafanua dhana hii kwa kupanua wigo na kujumuisha masuala mengi. Kwa mfano, Michel Foucault anadai kuwa kilongo ni mfumo mpana unaojumuisha mamlaka na ushawishi vinavyoathiri maarifa, imani na mitazamo ya kipindi fulani cha kihistoria (Paz, 2013). Miongoni mwa athari ya utelezi wa fasili za kilongo ni kutofautiana kwa mbinu na mielekeo ya uchambuzi wake (Wodak, 2011; Taylor, 2014). Wodak anaeleza kuwa kilongo ni muktadha wa utumiaji wa lugha ya mazungumzo au maandishi. Kwa maneno mengine, kilongo ni mwenendo wa jamii. Kilongo kama mwenendo wa kijamii unajumuisha uhusiano baina ya miktadha ya utokeaji wa tukio, hali inayotawala, taasisi, na miundo ya kijamii ambayo inazunguka tukio hilo. Wodak (2014) anaendelea kusisitiza kuwa ingawa muktadha wa utokeaji wa tukio unaathiriwa na vipengele hivyo, muktadha husika unaviathiri vipengele hivyo pia.

Kwa mujibu wa Fairclough (1992a), kilongo ni mienendo ya kijamii inayounda mitazamo ya kijamii, utambulisho, maarifa na mifumo ya maarifa. Katika muktadha wa makala haya, kilongo ni jumla ya vipengele vyote muhimu vinavyotawala na kufanikisha mawasiliano ya kawaida au ya kisanaa katika muktadha wa kijamii. Baadhi ya vipengele hivyo ni matini[3], utambulisho, utamaduni, vipengele vya kimasilugha, muktadha wa mawasiliano, violezi, tukio linalotawala na lile linalohusika katika mada ya mawasiliano. Aidha, vipengele hivi sharti vitazamwe kwa kuhusisha wawasiliani pamoja na hali na sifa zao. Baada ya kutoa ufafanuzi huo mfupi wa dhana ya kilongo, sehemu inayofuata inaelezea kwa muhtasari dhana ya uchambuzi kilongo.

### 3.2 Uchambuzi Kilongo


Fasili ya uchambuzi kilongo inahusiana na dhana ya kilongo. Kwa ufupi, uchambuzi kilongo ni uchanganuzi wa matini kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya kimuktadha vinavyohusiana na matini hiyo (Brown na Yule, 1983; Cook, 2005). Ni uchambuzi wa maana unaotoa uzito katika vipengele mbalimbali vilivyo nje ya mipaka ya sentensi. Kama inavyosisitizwa na Sara Mills (2024) kwamba uchambuzi kilongo ni uchanganuzi wa maana unaokinzana na misingi ya kawaida ya kiisimu inayochambua maana kwa kuzingatia viambajengo na maumbo mbalimbali katika sentensi. Kwa hiyo, maana ya matini inakamilika inapowekwa katika muktadha wake wa utendaji ambao unajumuisha vipengele vingi zaidi, hususani wahusika, jamii na maisha kwa ujumla kama inavyosisitizwa na Stephanie Taylor kwamba, uchambuzi kilongo "[ni] uchunguzi wa kina wa

[3] Matini inaweza kuwa kitu au alama yoyote kama vile maandishi, mazungumzo, mchoro au mchoro na ishara yoyote inayofanikisha mawasiliano katika kikundi fulani cha watu (taz. Hanks, 1989; Wodak, 2011).

lugha na matumizi yake kama ushahidi wa vipengele vya jamii na maisha kwa ujumla" (Taylor, 2014: 4). Kwa hiyo, lugha au matini yoyote nyingine ni kama kiwakilishi cha masuala mengi yanayoendelea katika jamii, kwa namna ya pekee namna lugha inavyodokeza mahusiano ya kimamlaka katika jamii. Kama ilivyo katika fasili ya kilongo, hakuna aina moja ya mkalaba wa uchambuzi kilongo. Ndiyo maana katika kitabu cha *Analysing Discourse*, Fairclough (2003) amebainisha aina mbili za mikabala, yaani mkabala unaochambua matini kwa kina na mikabala ambayo haikiti msingi wake katika uchambuzi wa matini. Uchambuzi kilongo ni uchanganuzi wa matini unaozingatia maudhui ya matini kwa kuzingatia miundo midogomidogo ya lugha ndani ya matini, utendaji wake na muktadha wa kijamii. Kwa maneno mengine, uchambuzi kilongo ni uchambuzi wa lugha katika muktadha wa matumizi yake katika jamii katika kipindi fulani maalumu; na ndiyo maana, mchambuzi kilongo anamakinikia zaidi uhusiano wa matini na mwandishi au mzungumzaji badala ya uhusiano wa vipashio mbalimbali ndani ya matini pekee (Brown na Yule, 1983). Maana ya matini inakamilishwa na taarifa za kimuktadha.

Nadharia hii imetumiwa katika makala haya kwa sababu matini teule imewasilishwa kwa namna ambayo inahitaji kuchambuliwa kwa kuzingatia mamlaka na ushawishi. Mtindo wa msanii kuzungumza na Korona ni wa kipekee ikilinganishwa na nyimbo nyingine za hamasa katika mapambano dhidi ya UVIKO-19. Lugha inayotumiwa katika mazungumzo hayo inadokeza uhusiano wa kimamlaka baina ya pande hizo mbili, suala mojawapo la msingi katika uchambuzi kilongo (Van Dijk, 2013; Fairclough, 2015). Aidha, masuala mengi katika matini hiyo yanaweza kueleweka kwa kuzingatia muktadha wa utendaji na vipengele vingine vilivyo nje ya matini husika.

Uchambuzi wa matini teule utatumia mkabala wa uchambuzi kilongo wa Norman Fairclough unaojumuisha ngazi tatu ambazo ni: (i) matini (ii) mienendo ya utendaji wa matini, na (iii) mienendo ya kijamii. Kwa mujibu wa Fairclough (1992a:72), dhana ya ngazi tatu za uchambuzi wa kilongo ni jaribio la kutumia uchambuzi unaojumuisha mikabala ya aina tatu muhimu ya uchambuzi ambayo ni: (i) uchambuzi wa kina wa matini kwa misingi ya kiisimu (ii) mkabala wa uchambuzi wa kimakrososholojia ambao unajumuisha mienendo ya kijamii na mifumo ya kijamii, na (iii) mkabala wa kimikrososholojia ambao unazingatia mienendo ya kijamii kama matokeo ya matendo na taratibu za kijamii. Kielelezo Na. 1 kinaonesha kiunzi cha uchambuzi wa ngazi hizo.




**Kielelezo Na. 1:** *Kiunzi cha Uchambuzi Kilongo*

Mwanazuoni huyu anaeleza kuwa mchambuzi kilongo anaweza kuanzia katika hatua yoyote katika kiunzi hicho kulingana na aina ya matini na namna anavyoona inafaa (Fairclough, 1992a). Katika makala haya, ingawa hatua ya awali itajikita katika uchambuzi wa matini, mara kwa mara, hatua ya utendaji matini na mienendo ya kijamii zitakuwa zinajumuishwa pale inapofaa. Katika hatua ya uchambuzi matini, maana za msingi za matini, miundo, uelekezi na nafsi za vitenzi zitabainishwa kama inavyoelezwa katika sehemu inayofuata.

## 4.0 Uchambuzi wa Matini

Katika makala haya, uchambuzi umeanza na uchanganuzi wa matini na kumalizia na muktadha wa kijamii. Hata hivyo, ufafanuzi unaweza kuvuka mipaka ya ngazi husika pale inapohitajika ili kurahisisha fasiri za data.

## 4.1 Uchambuzi wa Matini Teule

Uchambuzi wa matini unazingatia vijenzi vidogovidogo vya matini vinavyounda vijenzi vikubwa ambavyo vinatoa maudhui ya jumla ya matini (Van Dijk na Kintsch, (1983). Katika uchambuzi wa matini, vipengele vifuatavyo vilichanganuliwa: aina ya maswali yanayoulizwa, utolewaji wa masharti na wigo wa utekelezaji wa masharti, lugha ya dharau na chuki dhidi ya UVIKO-19, nafsi ya wingi, ukimya wa Korona na mwingilianomatini.

### 4.1.1 Matumizi ya Maswali

Matini teule ina maswali makuu matano ambayo ni:

(i) Korona wewe ni nani?
(ii) Umekuja kwa ajili ya nani?
(iii) Je, tukuchinjie jogoo wetu au utaondoka?
(iv) You know what?
(v) Kwenye mahaba na mapenzi je?

Maswali hayo yana maudhui tofauti. Swali la kwanza, "Korona wewe ni nani?", linahusu utambulisho. Katika hali ya kawaida, swali hili linatarajiwa kuulizwa kwa mtu ambaye hajulikani. Linapoulizwa kwa mtu anayejulikana, swali hili linaashiria kitu kingine. Si tena kuhitaji taarifa bali kudadisi namna mamlaka yanavyotumiwa vibaya. Swali linataja jina la "Korona", maana yake si suala la kujua utambulisho bali kudadisi suala lingine. Ikumbukwe kuwa swali hili linaanza baada ya kiitikio kinachomtaka Korona afunge virago. Kwa mantiki hiyo, swali la kwanza linahoji uhalali na mamlaka ya Korona kuingia bila ruhusa katika jamii. Hata hivyo, umuhimu wa swali hili upo katika uhusiano wa anayeuliza na anayeulizwa swali. Kwa kawaida, swali kama hili linaashiria dharau kwa anayeulizwa kutokana na kujichukulia mamlaka asiyostahili. Muulizaji anajua jina, anajua hatari za Korona na anajua namna ya kumdhibiti Korona. Kwa hiyo, anamjua Korona vizuri sana. Kwa mantiki hiyo, swali linalenga kudadisi matendo ya Korona yanayovuka mamlaka yake kama kirusi. Swali hili linaidhalilisha Korona kwa sababu imejichukulia mamlaka sehemu ambayo inaelekea kumdhalilisha.

Swali la pili, "Umekuja kwa ajili ya nani?" linahoji dhamira ya Korona. Kama swali la kwanza, swali hili linaulizwa katika muktadha ambapo mwenyeji hataki kumpokea mgeni. Katika utamaduni wa Waswahili na Waafrika kwa ujumla, mgeni hukaribishwa kwanza, kisha malengo ya ujio wake huulizwa baadaye. Uulizaji wa namna hii unadokeza masuala mawili: mosi, mshangao wa mgeni anayekuja bila taarifa na zaidi ni mgeni anayeenda sehemu ambayo hajulikani au hakubaliki. Swali hili pia linadokeza chuki dhidi ya mgeni. Swali la "Umekuja kwa ajili ya nani?" linaonesha kuwa mtu anayeuliza hamtaki mgeni. Kwa hiyo, maswali haya mawili yanaonesha chuki dhidi ya kirusi cha Korona. Aidha, maswali haya huulizwa mtu mwenye uwezo duni. Haitarajiwi mgeni au mvamizi mwenye uwezo mkubwa kuulizwa maswali kama haya. Jambazi ambaye ana silaha nzito hawezi kuulizwa maswali kama haya, badala yake yeye ndiye anayetoa amri.

Swali la tatu, "Je, tukuchinjie jogoo wetu au utaondoka?" linamtaka Korona ajitathmini kama kweli anapaswa kuchinjiwa jogoo kama sharti la kukubali kuondoka Tanzania au aondoke mwenyewe bila sharti lolote kutokana na sifa za Watanzania wanapoamua kupambana. Jogoo ni ndege dume wa jamii ya kuku ambaye anahusishwa na masuala mengi kama vile urijali, ubabe na utawala, sifa zinazompa thamani kubwa katika jamii. Yumkini ndiyo sababu inayomfanya awe kitoweo cha heshima katika jamii. Kutokana na thamani yake, jogoo huhusishwa na miviga ya aina mbalimbali barani Afrika (taz. Mellott, 1984; Olupona, 1993; Christensen, 2015). Swali hili ni kejeli kwa Korona kwani hadhi yake kwa Watanzania si ya kustahili kuchinjiwa jogoo, ndege mwenye thamani kubwa. Kwa maneno mengine, Korona aondoke mwenyewe kwani kwa usuli aliofafanuliwa kuhusu Watanzania alipaswa kujua kuwa angeondoshwa tu hata bila kuchinjiwa kuku. Ili asiendelee kujidhalilisha, anaonywa afadhali aondoke. Swali hili

linaulizwa baada ya kufafanua historia ya taifa la Tanzania na viongozi wake shupavu walivyofanikiwa kupambana na maadui mbalimbali:

> *Kumbuka Korona,*
> *Wewe ni Kidudu tu,*
> *Tena mmoja!*

Korona anaoneshwa kuwa hawezi kuwa tishio kwa taifa la Tanzania. Suala hili linadhihirika kwa msisitizo wa kirai, "Tena mmoja!" yaani watu walioungana hawawezi kushindana na "kidudu" kimoja. Kwa mara nyingine tena, msanii anaonesha lugha ya dharau kwa Korona na kudokeza kuwa si ugonjwa unaopaswa kuwa tishio kwa taifa ambalo lina dhamira ya kupambana na maradhi haya. Swali linaloenda sambamba na hilo limeulizwa kwa Kiingereza, "You know what?" Swali hili la Kiingereza limeulizwa ili kuweka msisitizo wa taarifa inayofuata ambayo labda Korona hajawahi kuisikia kuwa kuna adui alishadhibitiwa ndani ya muda mfupi sana. Kwa ujumla, maswali yote yanaelekea kumtisha Korona na kuonesha kuwa Watanzania wana uwezo mkubwa hata kama wao wenyewe hawalitambui hilo.

Swali la mwisho linahusu changamoto kubwa ya kupambana na Korona katika mahusiano ya kimapenzi ambapo kanuni nyingi za kupambana na UVIKO-19 haziwezi kufanya kazi. Inaonekana kuwa kuna changamoto kubwa ya kupambana na maradhi haya katika mahaba ambapo kanuni zake nyingi zinapaswa kuvunjwa ili kukamilisha matendo ya mapenzi. Kwa maneno mengine, msanii anaonesha kuwa pamoja na kufanikiwa kuudhibiti ugonjwa huu kuna maeneo ambayo yana changamoto kubwa, ndiyo maana hasemi chochote badala yake anamalizia, "Kwenye mahaba na mapenzi je? Korona, Korona angalia ooh!"

Kwa ujumla, maswali yaliyoulizwa katika matini hii yana dhima kuu mbili, mosi, kudhihirisha ukubwa wa taifa la Tanzania na nguvu waliyonayo Watanzania katika kupambana na Korona, na pili, kubainisha changamoto kubwa ambayo haionekani kupata suluhu yake haraka.

### 4.1.2 Masharti na Wigo wa Utekelezaji wake

Katika mazingira ya kawaida, anayetoa masharti au anayetawala na kudhibiti mawasiliano katika muktadha fulani ni yule mwenye mamlaka (Van Dijk, 2013; Fairclough, 2015). Mwenyeji mwenye nguvu anaweza kutoa masharti kwa mgeni. Mwenyeji dhaifu hana namna ya kutoa masharti kwa mgeni mwenye uwezo zaidi yake. Ndiyo maana kuna msemo katika Kiswahili usemao, 'mwenye nguvu mpishe'. Matini inaonesha mwenyeji ana uwezo na anatoa masharti kadhaa kwa mgeni. Sharti kubwa linadhihirika katika swali hili: "Unahitaji nini tukupe uondoke?" Hii ni lugha ya kejeli, dhihaka na jeuri inayomaanisha kuwa Korona, "mgeni", hatakiwi kuishi katika jamii na anaambiwa kwa mamlaka. Korona si tishio kubwa kwa taifa kama wengi walivyoihofia. Mpoto anasisitiza kuwa jamii

ipo tayari kutumia mali zake zenye thamani kubwa zilizopangiwa matumizi mengine muhimu ili kupambana na ugonjwa huu, hususani pale anaposema:

*Unahitaji nini tukupe uondoke,*
*Tuko tayari kukuchinjia jogoo,*
*Tuliyemweka kwa ajili ya mbegu.*

Pamoja na kuudogosha, kauli hizi zinadhihirisha kuwa Korona ni ugonjwa hatari ambao unapaswa kudhibitiwa kwa mapambano makali, ikiwamo kubadilisha vipaumbele vilivyowekwa na serikali. Uwezo wa kufanya hivyo nchini Tanzania upo.

#### 4.1.3 Matumizi ya Lugha ya Dharau, Chuki na Vitisho

Msamiati uliotumiwa katika kuwasiliana na Korona unabainisha hisia za chuki, dharau na vitisho. Aina ya kilongo kinachotumiwa kwa kawaida kinaweza kubainisha mwelekeo wa kihisia na kinidhamu alionao msemaji kwa msikilizaji (Van Dijk, 2013). Katika matini ya wimbo huu, hisia hizo zinajitokeza waziwazi katika nafasi mbalimbali.

Mstari wa kwanza wa kiitikio cha wimbo huo unadokeza hisia hizo za dharau na chuki dhidi ya Korona. Mstari wa kwanza una maneno yafuatayo: "Korona funga virago utuache salama...". Kirai "funga virago" ni nahau inayoonesha dharau na hisia za chuki. Miongoni mwa wazungumzaji wa Kiswahili, kauli hii "funga virago" inaashiria kuondolewa katika mji wa mtu au nchi bila heshima. Ni lugha inayotumiwa mtu anapofukuzwa au kuondolewa kwa namna isiyo na staha. Kwa kawaida, dharau huoneshwa kwa mtu ambaye yupo chini kimamlaka. Kwa mtu anayetisha na mwenye mamlaka makubwa hawezi kutamkiwa maneno hayo. Mbinu hii inatumiwa kama nyenzo ya kuhamasisha watu kuondokana na woga na unyonge, badala yake kujipa ujasiri wa kuushinda ugonjwa huu. Aina hii ya ushairi wa kuhamasisha watu hutumiwa vitani ili kuwatia moyo wapiganaji (taz. Chiwome, 1990; Wilson Jr., 2006; Nuxoll, 2014). Kutokana na vita kuhusisha mapigano na mauaji, wapiganaji huingiwa na hofu wakati mwingine, nyimbo za hamasa husaidia kuondoa woga na kuongeza ujasiri.

Aidha, msanii anadhihirisha chuki yake dhidi ya maradhi ya UVIKO-19 ambayo yamewekwa kisanii kama mvamizi. Kwa mujibu wa Fortuna na Nunes (2019), lugha chukizi ni ile inayoshambulia au kudhalilisha, inayochochea vurugu au chuki dhidi ya makundi ya watu kutokana na sifa za kimwonekano, kidini, kimbari, kitaifa n.k., inayotokea kwa mitindo bayana au ya ucheshi. Harris na wenzake (2022) wanadai kuwa lugha chukizi ni lugha kali, yenye kuumiza, mbaya na inayolenga kudunisha watu wengine. Wakati Fortuna na Nunes wanatazama kwa upande wa mtoaji wa lugha, Harris na wenzake wanatazama kwa upande wa mwathirika. Kwa ujumla, lugha ya chuki ni lugha ya kuudhi, inayotolewa kwa mitindo mbalimbali yenye lengo la kudhalilisha au kuibua hisia za chuki dhidi ya

mtu au kundi fulani la watu ili wahisi kuwa hawana hadhi sawa na wengine au mienendo yao haikubaliki katika jamii wanayoishi.

Vilevile, lugha ya vitisho imetumika ili kumwonesha Korona kuwa hana uwezo wa kuwatisha Watanzania. Kwa kawaida, lugha ya vitisho hutolewa kwa msikilizaji ambaye uwezo wake unafahamika kwa mtishaji. Vitisho hutumiwa kama silaha ya kupambana na adui. Kwa mfano, katika ubeti huu inaelezwa:

*Unahitaji nini tukupe uondoke,*
*Tuko tayari kukuchinjia jogoo,*
*Tuliyemweka kwa ajili ya mbegu.*
*Lakini kabla ya kumla jogoo wetu,*
*Tukujulishe sisi ni akina nani,*
*Ukoo wa nani,*
*Ili tusije kulaumiana siku za usoni.*

Kauli kwamba "Lakini kabla ya kumla jogoo wetu, Tukujulishe sisi ni akina nani, Ukoo wa nani, Ili tusije kulaumiana siku za usoni" ni lugha ya vitisho. Vitisho hivi vinamtahadharisha Korona kuwa anapambana na jamii ambayo huenda haijui vizuri, ndiyo maana msanii anamalizia kwa kusema, "Ili tusije kulaumiana siku za usoni". Hivi vyote ni vitisho kuwa Watanzania wana historia ya ushindi. Hawashindwi kirahisi. Kwa hiyo, hata katika vita hivi, hawatashindwa watakapoamua kupambana. Korona anapewa angalizo kuwa asikimbilie kuomba apewe nini badala yake ajitathmini vizuri kama kweli anahisi atapata anachokitaka. Vitisho hivyo ambavyo ni majigambo, vinaendelea kutolewa:

*Korona sisi ni Vitanzania,*
*Wajukuu wa Nyerere,*
*Tunaoongozwa na jemedari wetu Magufuli*
*Timu ya ushindi.*
*Kuna makabila mia moja na ishirini,*
*Watu milioni hamsini na nane.*
*Kumbuka Korona,*
*Wewe ni kidudu tu,*
*Tena mmoja.*

Vitisho vinatolewa kwa kutaja mashujaa wanaojulikana katika jamii. Hii ni sifa kubwa katika majigambo ambapo mashujaa hutajwa ili kuihamasisha jamii na kuamsha ari ya mapambano. Mashujaa wanaotajwa katika wimbo huu ni Nyerere, ambaye ni Baba wa Taifa na Magufuli. Viongozi wote hawa wawili walijulikana barani Afrika kutokana na ujasiri na kusimamia uamuzi wao (taz. Mnenuka, 2022). Aidha, msanii anaendelea kueleza kuwa Watanzania wapo milioni 58 kudhihirisha kuwa idadi hiyo ya watu ikiungana hakuna kinachoweza kushindikana. Msisitizo mkubwa zaidi umebainishwa katika mistari mitatu ya mwisho: "Kumbuka Korona, Wewe ni Kidudu tu, Tena mmoja!" Korona inadunishwa ili kuivunja moyo kuwa haitashinda kwa sababu kubwa mbili: mosi, Korona ni mdudu mdogo. Mbinu hii

ya kudharau upande unaotisha ni mbinu mojawapo ya kuongeza ujasiri wa kupambana na adui wa vita (taz. Różycki, 2021). Mchakato wa kunyambua nomino mdudu kutoka ngeli ya "M-" kwenda ngeli ya "Ki-" una dhima ya udunishaji (Schadeberg, 1984; Ndomba, 2022). Kwa hiyo, msanii anaposema ni kidudu anamaanisha ni mdudu mdogo. Aidha, matumizi ya kielezi "tu", yanaongeza msisitizo kuwa hadhi ya Korona inaishia katika ngazi hiyo duni ya "kidudu". Haina hadhi nyingine yoyote ya ziada. Kama ni mdudu tu hawezi kuwasumbua binadamu. Kwa hiyo, haiwezi kuwa tishio kwa "sisi" na kwa namna yoyote "sisi" tulio wengi tutashinda.

Vilevile, msanii anamalizia kwa kubainisha kuwa siyo tu kuwa "sisi" ni wengi bali ni wamoja. Idadi kubwa ya watu inapoungana inakuwa silaha kubwa katika mapambano. Kwa mfano inaelezwa:

*Sisi ni wamoja,*
*Wenye uzalendo,*
*Utaifa ndani yetu.*
*Linapokuja janga kama la ujio wako,*
*Tunakuwa kitu kimoja,*
*Tunaungana!*
*Je, tukuchinjie jogoo wetu au utaondoka?*

Siri kubwa ya mafanikio ya Watanzania ni umoja, hasa pale jamii inapokumbwa na janga fulani (taz. Otieno, 2021). Baada ya kutoa vitisho, msanii anauliza, "Je, tukuchinjie jogoo wetu au utaondoka?" ili kubaini ikiwa bado kirusi cha Korona kinafikiri kwamba kinaweza kupambana au kiondoke chenyewe. Vitisho hivi vinahamasisha wasikilizaji wajione kuwa wana nguvu, umoja na wanaweza kuvishinda vita.

Pamoja na masuala mengine, heshima, dharau, furaha, huzuni na hisia nyingine hubainishwa kwa uteuzi wa msamiati. Wataalamu mbalimbali wa semantiki na isimujamii wanadai kuwa uteuzi wa msamiati unasaidia kubainisha utambulisho na uhusiano baina ya wawasiliani (Gumperz na Cook-Gumperz, 1982). Kuna lugha ya heshima ya kumueleza mtu aondoke sehemu fulani na kuna lugha isiyo na staha. Matumizi ya lugha hiyo yanategemeana na uhusiano na muktadha uliopo. Lugha itumiwayo na msanii inadhihirisha kuwa Korona, pamoja na kutisha kwake, si mhusika anayestahili heshima bali anapaswa kuelezwa kama mvamizi asiye na nidhamu. Kwa hiyo, lugha ya chuki, dharau na ya vitisho imetumiwa ili kuweka msisitizo kuwa mgeni huyu hapaswi kuogopwa wala hastahili kupewa heshima.

### 4.1.4 Matumizi ya Nafsi ya Kwanza Wingi

Lugha iliyotumiwa katika wimbo huu imetumia nafsi ya wingi. Kwa kawaida, matumizi ya nafsi ya wingi yanalenga kuonesha kuwa suala linalozungumzwa linajumuisha sauti ya wengi, na mzungumzaji hufanya hivyo kwa kuwakilisha

watu wengine. Katika muktadha wa wimbo huu, nafsi ya wingi imetumiwa kwa lengo kuu moja, yaani kuonesha kuwa Watanzania wapo pamoja na umoja wao ni nyenzo ya mafanikio ya kupambana na UVIKO-19. Umoja huu unabainishwa kwa namna kadhaa kama vile kuzungumza yale yanayoisibu jamii nzima, yaani kueleza kero na namna ya kupambana na adha ya Korona, kueleza bayana kuwa ili kufanikiwa katika vita dhidi ya Korona, kuna ulazima wa kuwa wamoja, na mwisho, matumizi ya nafsi ya kwanza wingi yanabainisha kuwa "sisi" tupo tofauti na "yeye" au "wao". Wazo hili linasisitizwa pia na Íñigo-Mora (2004) kuwa nafsi ya kwanza wingi ina dhima kadhaa kama vile kujumuisha au kutenga katika kundi. Katika muktadha wa makala haya, matini haimaanishi tu kuwa "Sisi, Watanzania", tupo tofauti na "yeye" Korona ambaye kwa hakika ni adui yetu bali tunapaswa kupambana na yeye kwa sababu anahatarisha maisha yetu. Kauli kadhaa zinajumuisha dhana ya wingi na umoja, kwa mfano:

*Tukujulishe* ***sisi*** *ni akina nani*
*Korona* ***sisi*** *ni Vitanzania*
***Sisi*** *ni wamoja*
*Wenye uzalendo*
*Utaifa ndani* ***yetu***
*Linapokuja janga kama la ujio wako*
***Tu****nakuwa kitu kimoja*
***Tu****naungana!*
***Sisi*** *ni wamoja vita* ***tu****taishinda pamoja Tanzania*

Mfano huu unaonesha matumizi ya nafsi ya kwanza wingi kama inavyoonekana katika kiwakilishi huru cha nafsi ya kwanza wingi *sisi* pamoja na kiambishi cha nafsi ya kwanza wingi {tu-} katika vitenzi *tu-kujulishe*, *tu-nakuwa* na *tu-naungana*. Matini hii inaonesha msisitizo wa kuwa na umoja katika mapambano dhidi ya kirusi huyu kama ilivyokuwa katika nyakati mbalimbali tangu enzi za Mwalimu Nyerere (taz. Otieno, 2021). Wimbo huu unadhihirisha ujumbe wa methali ya Kiswahili isemayo 'umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu'; kwamba katika janga hili, Watanzania wanapaswa kuwa wamoja. Kwa mujibu wa Fulton (2003), nafsi ya kwanza wingi ina dhima ya kuleta umoja na kudokeza sauti moja kwa makundi mbalimbali yaliyomo. Aidha, matumizi ya "sisi" yanadokeza ufanano wa kijamii. Ni nyenzo mwafaka ya kisiasa ya kuwaunganisha watu. Katika muktadha wa makala haya, nafsi ya wingi imetumiwa ili kuhamasisha umoja katika vita dhidi ya Korona kwa sababu pamoja na kuwa na jamii nyingi, dini mbalimbali, misimamo tofauti ya kisiasa na kijamii, kulikuwa na suitafahamu kadha wa kadha kuhusu namna sahihi ya kupambana na maradhi haya. Kwa hiyo, matumizi ya nafsi ya kwanza wingi yanalenga kuhamasisha umoja katika mapambano dhidi ya UVIKO-19.

### 4.1.5 Ukimya wa Korona

Katika wimbo huu, sauti ya Korona haisikiki pamoja na Korona kuelezwa masuala mbalimbali vikiwamo vitisho, majigambo na lugha ya dharau ya kuambiwa aondoke. Hata hivyo, mwangwi wa sauti yake unasikika kupitia vitisho vyake kama inavyoonekana hapa chini:

*Corona, umesimamisha dunia!*
*Sio kama hatuoni!*
*...*
*Corona watu hawalali wanakuwaza wewe tu!*
*"Nataka niwakute kwa wingi"*
*...*
*"Nitawapata kwenye salamu za mikononi"*

Maneno machache tu yanazungumzwa na Korona tena hayatumii lugha ya moja kwa moja. Maneno hayo machache, licha ya vitisho vingi, ni yale yanayoelezea namna ya kuwaathiri binadamu. Msanii amemkata ulimi mhusika Korona ingawa anaelezwa maneno makali sana. Mara nyingi, upande wenye nguvu una kawaida ya kusikika wenyewe tu huku ukiukata kauli upande mwingine (Glenn, 2004). Kwa hiyo, yumkini kwa kuwa tayari hadhi ya Korona kuwa ni kidudu imeshadunishwa, kinanyimwa nguvu ya kuzungumza kwa sababu hakina hadhi ya kuzungumza na binadamu. Vilevile, ukimya wa kirusi huyu unaweza pia kuashiria hatari aliyo nayo kwa binadamu (Watanzania), ndiyo maana kunasisitizwa kutolewa tahadhari ya kupambana naye. Kwa upande mwingine, ukimya wa Korona unaweza kudokeza namna ugonjwa huu unavyomwingia binadamu kimyakimya na kuishi katika mwili wake kwa siku kadhaa bila kujulikana huku binadamu akiendelea kuwaambukiza wenzake bila kujua. Wazo hili linakaribiana sana na dhana ya ukimya na usiri ilivyojadiliwa na Lemardelé (2013) kuwa ni dhana ambazo zinahusiana na wakati mwingine hutokea pamoja. Mwisho, ukimya huu unadokeza kuwa ugonjwa huu unaua. Dalili kubwa ya kifo kwa viumbe vingi ni kunyamaza kimya huku kukata kauli ikionekana kwa baadhi ya watu kuwa ni dalili mojawapo za kuelekea kufa. Uhusiano wa ukimya na kifo umeelezwa katika miktadha mbalimbali na Ephratt (2008). Yumkini ukimya wa Korona unaonesha kuwa ugonjwa huu hauzungumzi badala yake unatenda kimyakimya. Hivyo, tahadhari ni muhimu sana katika kupambana na adui ambaye hasikiki.

### 4.1.6 Mwingilianomatini

Mwingilianomatini ni istilahi iliyoundwa na Julia Kristeva ikitumia msingi wa usemezano wa mwanazuoni Mikhail Bakhtin (Pechey, 2007; Orr, 2011). Kwa mujibu wa Kristeva (1986), dhana ya usemezano inamaanisha matumizi ya matini zilizotumiwa na wengine, yaani hata katika monolojia kuna usemezano kwa sababu matini zinazotumiwa zimechukuliwa kutoka kwa wengine. Matini inapotumiwa katika muktadha fulani huchopolewa katika miktadha mingine,

haitoki moja kwa moja katika msamiati wa lugha ulio nje ya muktadha fulani kama inavyosisitizwa na Kristeva anaposema, "Istilahi hii 'mwingiliano' inamaanisha uchopekaji wa historia (jamii) katika matini na matini katika historia" (Kristeva, 1986: 39). Umuhimu wa mwingilianomatini katika uchambuzi kilongo unatokana na dhana kuwa uchambuzi kilongo unatumia matini katika muktadha wake; na matini hizo ndizo zenye mseto wa matini mbalimbali ambazo zinaweza kuwa bayana au zisiwe bayana kwa wasomaji tofauti kiasi cha kuathiri tafsiri hizo za matini (Fairclough, 1992a; 1992b). Ndiyo maana dhana ya mwingilianomatini ni muhimu katika uchambuzi kilongo.

Katika makala haya, kumejitokeza mwingilianomatini kwa kiasi kikubwa. Mosi, historia ya nchi ya Tanzania ambayo inajumuisha Rais wa Awamu ya Kwanza, Mwalimu Julius K. Nyerere, na kauli kadhaa alizozitoa zikiwapo za kuwatangaza maadui wakubwa watatu ambao ni ujinga, maradhi na umaskini. Pia, kumetumika matini kutoka katika hotuba ya Nyerere kuhusu sababu za kuingia vitani na serikali ya Uganda iliyokuwa chini ya Idd Amini Dada pale anaposema, "Tulimtandika asubuhi na mapema, maana sababu na utayari tulikuwa nao". Vilevile, msanii amemtaja John Pombe Magufuli kama kiongozi wa mapambano. Mapambano yanayoelezwa hapa ni yale yaliyofanyika dhidi ya ufisadi. Dhana hiyo ya kupambana na ufisadi imechopekwa katika muktadha wa mapambano ya Korona. Kwa ujumla, haya yote yanagusia historia ya Tanzania ambayo inadhihirisha ujasiri wa viongozi hao wawili, yaani Nyerere na Magufuli (taz. Fouere, 2019; Mnenuka, 2023). Mamlaka ya lugha iliyotumiwa na Nyerere wakati akitangaza vita dhidi ya majeshi ya Uganda imechopekwa katika muktadha wa dayalojia na Korona. Mamlaka hiyo imekuwa na umaarufu mkubwa zaidi kwa sababu Tanzania ilivishinda Vita vya Kagera. Vilevile, katika matini husika kumetumiwa taarifa mbalimbali zinazohusiana na maradhi ya UVIKO-19 pamoja na taratibu zake za kujikinga kama vile kuepuka mikusanyiko na kunawa kwa maji tiririka na sabuni.

Kwa ujumla, sehemu hii imemakinikia uchambuzi wa matini katika ngazi ya kwanza ya uchambuzi. Sehemu inayofuata inahusu utendaji wa matini, yaani matini teule imewasilishwa namna gani na imepokelewaje na hadhira na kwa kutumia njia zipi?

### 4.2 Utendaji wa Matini

Wimbo wa "Kwaheri Korona" ni kazi ya ushairi ambayo imetungwa na msanii kisha kurekodiwa studio na kusambazwa kwa njia mbalimbali kwa ajili ya kusikilizwa. Huu ni wimbo ambao unalenga kusikilizwa katika njia kadha wa kadha kama vile redioni, katika nyumba za starehe, katika vyombo vya usafiri na katika mitandaopepe mbalimbali ya kijamii kama vile *WhatsApp* na zaidi katika *YouTube*. Ingawa umepakiwa katika *YouTube,* wimbo huu hauna picha za video wala mkusanyiko wa picha. Kwa hiyo, hata yule anayeufungua katika mtandao

anasikiliza tu. Yumkini, kutokana na hali tete ya ugonjwa wenyewe, ujumbe wa sauti ulitosha kutoa elimu kwa umma. Aidha, kutokana na changamoto za fedha na kuhamasisha watu kukaa nyumbani, huenda kutoa picha kungeonesha kuwa msanii hatekelezi agizo hilo. Hadhira ya wimbo huu ni wasikilizaji katika redio, maeneo ya umma, nyumba za starehe, wasafiri na watumiaji wa mitandaopepe kama vile *WhatsApp* na *YouTube*. Katika utendaji huu, fanani na hadhira hawaonani ana kwa ana, lakini wimbo umeandaliwa kuifikia hadhira kubwa. Aidha, kutokana na hali ilivyokuwa, wimbo huu haukulenga kutumbuizwa katika hadhara ya watu kwa sababu nchini Tanzania, kama ilivyokuwa katika nchi nyingi duniani, mikusanyiko ya watu kwa ajili ya burudani ilizuiwa. Kwa hiyo, nyimbo zote zilizoimbwa katika kipindi hiki, hususani zile zilizotoa elimu kuhusu UVIKO-19 hazikutumbuizwa hadharani.

### 4.3 Muktadha wa Kijamii

Wimbo huu umeimbwa wakati ambapo woga dhidi ya UVIKO-19 umetanda nchi nzima kwa sababu ya idadi kubwa ya vifo vilivyosababishwa na UVIKO-19 nchini na ughaibuni. Habari kuhusu madhara ya ugonjwa huu zilianza kuenea majuma kadhaa kabla ya ugonjwa huu kubisha hodi nchini Tanzania. Idadi ya vifo katika nchi zilizoendelea kama vile Italia iliwashitua watu wengi sana wakiwamo wanasayansi. Hali hii ilitia hofu nchi nyingi zinazoendelea kwa sababu madhara yake yalitabiriwa kuwa makubwa zaidi barani Afrika kwa sababu ya huduma duni za afya, idadi kubwa ya maradhi nyemelezi huku miundombinu na suhula duni za kupambana na magonjwa ya milipuko ni duni (Lone na Ahmad, 2020; Nkengasong na Mankoula, 2020; Velavan na Meyer, 2020). Kwa hiyo, nyimbo nyingi zilijielekeza katika kuendeleza woga huu kama nyenzo ya kuhamasisha watu kujikinga na maradhi haya kwa kufuata kanuni za afya na pengine kusali ili kuomba msaada kwa Mungu. Kinyume na wasanii wengine, Mrisho Mpoto haendelezi woga wala haoneshi kuwa ugonjwa huu unatisha, badala yake anahamasisha juhudi za kupambana na ugonjwa huu bila woga kwa kuzingatia masharti yaliyotolewa na taasisi za afya ndani na nje ya nchi.

Kilongo cha woga kinageuzwa ili kufunua ukurasa mpya wa matumaini kwa kujenga ujasiri wa kupambana na UVIKO-19. Dhana iliyolengwa hapa ni ile ya kuondoa hofu dhidi ya ugonjwa huu, na badala yake kutumia mbinu na suhula zilizopo katika mapambano. Hili lilienda sambamba na tamko la aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John P. Magufuli, aliyewaasa Watanzania kupunguza hofu kwani inapunguza kinga. Aidha, katika wimbo huu, nguvu za kupambana na maradhi haya zimeelekezwa kwa binadamu (Watanzania) ambao wanaaswa kuweka dhamira ya kufuata masharti ya ugonjwa huu kama vile kunawa mikono kwa maji tiririka na kuepuka mikusanyiko kama njia pekee na rahisi ya kuudhibiti ugonjwa wa UVIKO-19. Wimbo huu ulihamasisha na kuwatia raia ujasiri wa kuamini kuwa uwezo na

nguvu za kuudhibiti ugonjwa huu vimo mikononi mwao wala si pahala pengine nje ya dunia yao.

Wimbo huu uliimbwa ili kuhamasisha uzalendo na uwajibikaji katika kupambana na UVIKO-19. Mzalendo anayelipenda taifa, mtu anayejihisi ni sehemu ya taifa lazima atafuata taratibu zote za kujikinga na ugonjwa huu ili asiwadhuru wengine na kuwezesha taifa liondokane na janga hili. Kwa mujibu wa BAKITA (2015:749), mzalendo ni "mtu anayeipenda nchi yake kwa moyo wake wote kiasi cha kuwa tayari kuipigania". Katika matini teule, msanii amesisitiza suala la uzalendo, umoja na utaifa. Akirejelea historia ya nchi, msanii ameonesha kuwa katika historia ya Tanzania, yaliwahi kutokea matatizo ambayo yalitatuliwa kwa sababu ya umoja, uzalendo na utaifa. Ikiwa raia anaipenda nchi yake kiasi cha kuwa tayari kuipigania, kwa vyovyote vile, katika janga hili la UVIKO-19, angekuwa mstari wa mbele kwa kufuata miongozo iliyotolewa na wataalamu wa afya ili kuhakikisha kuwa maradhi yanayosababishwa na virusi vya Korona yanadhibitiwa. Kwa mujibu wa Zhai, Lu na Wu (2023), matatizo makubwa yanapoikumba jamii na kuzua taharuki, watu huungana kwa sababu ya woga na wasiwasi wa mtu binafsi kulikabili tatizo. Ndiyo maana hakukuwa na namna nyingine ya kukabiliana na Korona zaidi ya kuungana pamoja kama taifa. Halikadhalika, umoja na utaifa wa raia wa Tanzania ulipaswa kudhihirika katika kufuata taratibu za kudhibiti ugonjwa. Yeyote ambaye alilegalega alichukuliwa kuwa adui wa taifa kwa sababu anafanya vitendo vinavyostawisha maradhi haya ambayo yalipoteza nguvukazi ya taifa. Unyonge, woga na wasiwasi wa Watanzania dhidi ya ugonjwa huu vingeweza kuondolewa mapema sana ikiwa kila mmoja angekuwa mzalendo kwa kujali utaifa na kushirikiana na raia wengine ili kuutokomeza ugonjwa huu.

Wimbo wa "Kwaheri Corona" uliimbwa ili kuikumbusha jamii kuwa kila raia ana jukumu la kusimama kidete kulitetea taifa wakati wa matatizo. Katika wimbo huu, msanii anataja nyakati kadhaa na maadui kadhaa waliowahi kutangazwa kama tishio kwa nchi ya Tanzania. Kwa mfano, maadui watatu waliotajwa na Mwalimu Nyerere mara baada ya uhuru 1961 ni maradhi, ujinga na umaskini. Katika kipindi cha UVIKO-19, miongoni mwa maadui watatu waliotajwa na Mwalimu, yaani adui maradhi (UVIKO-19) ndiye aliyekuwa akiisumbua jamii. Jamii ilikumbushwa kupambana na adui huyu kwa ujasiri mkubwa. Aidha, jamii ilitiwa moyo kuwa kuna wakati iliweza kuishinda vita kubwa kwani "sababu na utayari tulikuwa nao" (Mpoto na THT, 2020). Kumbukumbu hii inaibuliwa kwa sababu katika kukabiliana na UVIKO-19, taifa lilikuwa na sababu; suala pekee lililosuasua labda ni ari, hamasa na utayari wa kupambana na ugonjwa huu. Utayari huo ulihusu kufuata taratibu za kupambana na maradhi haya ili kuliepusha taifa na hatari iliyolikabili.

Kuikumbusha jamii historia yake husaidia kuibua ari, uzalendo na utaifa (Rolston, 2010). Historia si tu maelezo kuhusu masuala yaliyopita bali kutumia maelezo ya matukio yaliyopita ili kupambana na changamoto zinazojitokeza hivi sasa na siku zijazo. Kurejelea masuala kadhaa yaliyopita, kuwataja baadhi ya maadui na kueleza matukio ya kushinda vita ni mkakati wa kuibua ari ya umoja, uzalendo na utaifa kwa jamii. Kwa kawaida, kumbukumbu zina dhima ya kuibua ari ya umoja na ujasiri ambayo ilihitajika sana katika kukabiliana na maradhi ya UVIKO-19 kutokana na woga na wasiwasi uliotanda si tu Tanzania bali Afrika na duniani kote. Wimbo huu unaitumia historia kuibua kumbukumbu za nyakati za shida na namna taifa lilivyofanikiwa kuvuka katika vipindi vigumu kutokana na umoja na ujasiri. Kwa hiyo, raia walikuwa wakiaswa kuwa historia inaonesha kuwa katika umoja na ujasiri taifa linaweza kupambana na adui yeyote. Ndiyo maana msanii anasema Korona ni mdudu tu, kamwe haiwezi kuwa tishio kwa taifa kubwa lenye historia kubwa ya kupambana na maadui kama Tanzania.

## 5.0 Hitimisho

Makala haya yalilenga kuchambua maudhui ya wimbo teule ulioimbwa wakati wa mlipuko wa maradhi ya UVIKO-19. Imeelezwa kuwa baada ya mlipuko huo, kulitungwa nyimbo nyingi lakini wimbo wa Mrisho Mpoto ulikuwa wa kipekee kwa sababu ulilenga kuihamasisha jamii iwe na ujasiri mkubwa badala ya kuendelea kuwa na woga. Kwa kutumia Nadharia ya Uchambuzi Kilongo ya Fairclough inayozingatia ngazi tatu za uchambuzi, imeelezwa kuwa mbinu ya majigambo na ushairi wa kivita vimekuwa chachu ya kuwatia ujasiri Watanzania walipokumbwa na woga mkubwa wa UVIKO-19. Aidha, wimbo huu umebainisha kuwa mtindo ni sehemu muhimu ya kufuma na kuchambua maudhui. Mtindo wa kuzungumza na Korona kwa kuidharau umerahisisha kueleweka kwa ujumbe wake na hasa kuongeza hamasa kwa Watanzania katika mapambano dhidi ya UVIKO-19. Mtindo, kama ilivyodokezwa hapo awali, hautengani na maudhui bali ni sehemu ya maudhui.

## Marejeleo


BAKITA (2015) "Mzalendo". Katika *Kamusi Kuu ya Kiswahili*, Toleo 3. Nairobi: Longhorn Publishers Limited. uk. 749.

Brown, G. na Yule, G. (1983) *Discourse Analysis*. Cambridge Textbooks in Linguistics. Cambridge: Cambridge University Press.

Bryant, L.O. (2005) "Music, Memory, and Nostalgia: Collective Memories of Cultural Revolution Songs in Contemporary China." *China Review*, Special Issue on Collective Memories of the Cultural Revolution, 5 (2): 151-75.

Čarkič, M. (1996) "On the Notion of Style". *Stylistyka,* 5: 332-36.

Chiwome, E. (1990) “The Role of Oral Traditions in the War of National Liberation in Zimbabwe: Preliminary Observations”. *Journal of Folklore Research,* 27 (3): 241-47.

Christensen, T.G. (2015) *An African Tree of Life*. Eugene, Oregon: Wipf and Stock Publishers.

Cook, G. (2005) *Discourse*. Nachdr. Language Teaching. Oxford: Oxford University Press.

Dijk, T.A. na Kintsch, W. (1983) *Strategies of Discourse Comprehension*. New York: Academic Press.

Ephratt, M. (2008) “The Functions of Silence”. *Journal of Pragmatics,* 40 (11): 1909-1938. https://doi.org/10.1016/j.pragma.2008.03.009.

Fairclough, N. (1992b) “Intertextuality in Critical Discourse Analysis”. *Linguistics and Education* 4: 269-93.

Fairclough, N. (2003) *Analysing Discourse: Textual Analysis for Social Research*. London: Routledge.

Fairclough, N. (1992a). *Discourse and Social Change*. Cambridge, UK; Cambridge, MA: Polity Press.

Fairclough, N. (2015) *Language and Power*. London: Routledge.

Fortuna, P. na Nunes, S. (2019) “A Survey on Automatic Detection of Hate Speech in Text”. *ACM Computing Surveys* 51 (4): 1–30. https://doi.org/10.1145/3232676.

Fouere, M. (2019) “Commemorating Nyerere, Celebrating Magufuli in Tanzania”. hal-02510080. Inapatikana katika https://hal.science/hal-02510080/document. Ilisomwa tarehe 01 Januari 2024.

Fulton, D. (2003) “‘Romans Des Nous’: The First Person Plural and Collective Identity in Martinique”. *The French Review*. Special Issue on Martinique and Guadeloupe, 76 (6): 1104–14.

Glenn, C. (2004) *Unspoken: A Rhetoric of Silence*. Carbondale: Southern Illinois University Press.

Guardado, M. (2018) *Discourse, Ideology and Heritage Language Socialization: Micro and Macro Perspectives*. De Gruyter. https://doi.org/10.1515/9781614513841.

Gumperz, J.J. na Cook-Gumperz, J. 1982. “Introduction: Language and the Communication of Social Identity”. Katika J.J. Gumperz (Mh.) *Language and Social Identity,* Studies in Interactional Sociolinguistics 2. Cambridge: Cambridge University Press. 1-21.

Gunderson, F. (2010) *Sukuma Labor Songs from Western Tanzania: ‘We Never Sleep, We Dream of Farming’*. BRILL. https://doi.org/10.1163/ej.9789004184688.i-536.

Habib, R. (2022) “Arabic Songs: An Affective Forum for Combating COVID-19 and Other Insecurities”. *Text & Talk.* https://doi.org/10.1515/text-2021-0042.

Hamisi, N.M., Dai, B. na Ibrahim, M. (2023) "Global Health Security amid COVID-19: Tanzanian Government's Response to the COVID-19 Pandemic". *BMC Public Health* 23 (1): 205. https://doi.org/10.1186/s12889-023-14991-7.

Hanks, W.F. (1989) "Text and Textuality". *Annual Review of Anthropology* 18 Annual Reviews: 95-127. https://doi.org/10.2307/2155887.

Harris, C., Halevy, M., Howard, A., Bruckman, A. na Yang, D. (2022) "Exploring the Role of Grammar and Word Choice in Bias Toward African American English (AAE) in Hate Speech Classification". Katika *2022 ACM Conference on Fairness, Accountability, and Transparency*. Seoul: ACM. kur. 789-98. https://doi.org/10.1145/3531146.3533144.

Hendricks, W.O. (1980) "The Notion of Style". *Language and Style.* XIII (1): 35-54.

Herrmann, J.B., Dalen-Oskam, K. na Schöch, C. (2015) "Revisiting Style, a Key Concept in Literary Studies". *Journal of Literary Theory* 9 (1). https://doi.org/10.1515/jlt-2015-0003.

Íñigo-Mora, I. (2004) "On the Use of the Personal Pronoun *We* in Communities". *Journal of Language and Politics* 3 (1): 27–52. https://doi.org/10.1075/jlp.3.1.05ini.

Kahigi, K. (1997) "Structural and Cohesion Dimension of Style: A Consideration of Some Swahili". *Journal of Linguistics and Language in Education,* 3: 1-77.

Kipacha, A. (2015) "The Blason Populaire in Swahili Paremia". *Proverbium* 32: 205-20.

Kristeva, J. (1986) "Word, Dialogue and Novel". Katika *The Kristeva Reader*, Toril Moi (Mh.), A. Jardiney, T. Gora, na L.S. Roudie (Wafasiri). New York: Columbia University Press. kur. 34-61.

Leech, G.N. na Short, M. (2013) *Style in Fiction: A Linguistic Introduction to English Fictional Prose*, English Language Series. London: Routledge.

Lemardelé, G. (2013) "Silence, Secrecy and Sacredness in Hardy's Fiction: The Example of Far from the Madding Crowd and Tess of the d'Urbervilles". *FATHOM*, Na. 2. https://doi.org/10.4000/fathom.358.

Lone, S.A., na Ahmad, A. (2020) "COVID-19 Pandemic - An African Perspective". *Emerging Microbes & Infections*. 1-28. https://doi.org/10.1080/22221751.2020.1775132.

Mellott, N. (1984) "Summaries of Sacrificial Rites Described in the Preceding Four Issues of Systèmes de Pensée En Afrique Noire". *Systèmes de Pensée En Afrique Noire* 6: 149-83. https://doi.org/10.4000/span.555.

Mills, S. (2004) *Discourse*. London: Routledge.

Mnenuka, A. (2023) "Dhima Za Umatinishaji-Upya katika Fasihi: Uchunguzi Kifani wa Nyimbo za Muziki wa Dansi na Ngano". *Kioo cha Lugha* 20 (2): 198-216. https://doi.org/10.4314/kcl.v20i2.4.

Mnenuka, A. (2024) "'Kuna Corona Fake na Og': The Role of Postcolonial Laughter during the COVID-19 Outbreak in Tanzania". *The African Review*, 1–26. https://doi.org/10.1163/1821889x-bja10075.

Mpoto, M. na THT. (2020) *Kwa heri Corona*. Unapatikana katika https://www.youtube.com/watch?v=utyHbLAcE6U. Ulitazamwa tarehe 28 Juni 2023.

Ndiaye, B., na Rowley, M. (2022) ""Mbas Mi": Fighting COVID-19 through Music in Senegal". *African Studies Review.* Juz. 65 (1): 234-59. https://doi.org/10.1017/asr.2021.115.

Ndomba, R.G. (2022) "Diminutive Noun Class in Bantu Languages: Is Kiswahili Deviant?" *Journal of Humanities and Social Sciences.* Juz. 11 (2): 1-17.

Nkengasong, J.N. na Mankoula, W. (2020) "Looming Threat of COVID-19 Infection in Africa: Act Collectively, and Fast". *The Lancet,* Juz. 395 (10227): 841-42. https://doi.org/10.1016/S0140-6736(20)30464-5.

Nuxoll, Co. (2014) "Borrowed Tunes. Commando and Morale Booster Songs of RUF Fighters in the Sierra Leone War". *Transposition*, Na. 4 (Juni). https://doi.org/10.4000/transposition.598.

Olupona, J.K. (1993) "Some Notes on Animal Symbolism in African Religion and Culture". *Anthropology and Humanism* 18 (1): 3-12. https://doi.org/10.1525/ahu.1993.18.1.3

Orr, M. (2011) "Intertextuality". Katika M. Ryan, G. Castle, R. Eaglestone na M.K. Booker (Wah.). *The Encyclopedia of Literary and Cultural Theory*, Malden, MA: Wiley-Blackwell. kur. 641-45

Otieno, S.D. 2021. "Archives of a Pandemic: Song and the Mitigation of the COVID-19 Pandemic in East Africa". *Cogent Arts & Humanities* 8 (1): 1946245. https://doi.org/10.1080/23311983.2021.1946245.

Paz, A.I. (2013) "Discourse Theory". Katika R.J. McGee na R.L. Warms (Wah.) *Theory in Social and Cultural Anthropology: An Encyclopedia*. Thousand Oaks, California: Sage Publications, Inc. kur. 191-96.

Pechey, G. (2007) *Mikhail Bakhtin: The Word in the World*. Critics of the Twentieth Century. London: Routledge.

Rolston, B. (2010) "'Trying to Reach the Future through the Past': Murals and Memory in Northern Ireland". *Crime, Media, Culture: An International Journal,* 6 (3): 285-307. https://doi.org/10.1177/1741659010382335.

Rosengren, I. (1972) "Style as Choice and Deviation". *Style*, 6 (1): 3-18.

Różycki, Ł. (2021) *Battlefield Emotions in Late Antiquity: A Study of Fear and Motivation in Roman Military Treatises. History of Warfare*, Juz. 136. Leiden: Brill.

Schadeberg, T.C. (1984) *A Sketch of Swahili Morphology*. Dordrecht: Foris Publishers.

Tarimo, C.S. na Wu, J. (2020) "The First Confirmed Case of COVID-19 in Tanzania: Recommendations Based on Lesson Learned from China".

*Tropical Medicine and Health.* Juz. 48 (25): https://doi.org/10.1186/s41182-020-00214-x.

Taylor, S. (2014) *What Is Discourse Analysis?* London: Bloomsbury.

Thompson, R.G.A., Nutor, J.J. na Johnson, J.K. (2021) "Communicating Awareness about COVID-19 Through Songs: An Example From Ghana". *Frontiers in Public Health* 8: 607830. https://doi.org/10.3389/fpubh.2020.607830.

Thornbury, S. (2010) "What Can a Corpus Tell Us about Discourse?" Katika A. O'Keeffe na M. McCarthy (Wah.) *The Routledge Handbook of Corpus Linguistics*. Routledge Handbooks in Applied Linguistics. London; New York: Routledge: 270-87.

Tyler, D. (2021) "On Style: An Introduction". Katika D. Tyler (Mh.) *On Style in Victorian Fiction.* Cambridge: Cambridge University Press. kur.1-20.

Van Dijk, T.A. (2013) "Discourse, Power and Access." Katika C.R. Caldas-Coulthard na M. Coulthard (Wah.) *Texts and Practices: Readings in Critical Discourse Analysis*. Abingdon, Oxon: Taylor and Francis. kur. 84-104.

Velavan, T.P. na Meyer, C.G. (2020) "The COVID-19 Epidemic". *Tropical Medicine & International Health* 25 (3): 278-80. https://doi.org/10.1111/tmi.13383.

Walpole, J.R. (1980) "Style as Option". *College Composition and Communication*, 31 (2): 205-212.

Wilson Jr., J.A. (2006) "Political Songs, Collective Memories, and Kikuyu Indi Schools". *History in Africa,* 33: 363-88.

Wodak, R. (2014) "Critical Discourse Analysis". Katika *The Routledge Handbook of English Studies*, C. Leung and B.V. Street (Wah.), 302-16. London: Routledge, Taylor & Francis Group.

Wodak, R. (2006) "Review: Dilemmas of Discourse (Analysis)". *Language in Society* 35 (4): 595-611.

Wodak, R. (2011) "Critical Linguistics and Critical Discourse Analysis". Katika J. Zienkowski, Östman, J. na Verschueren, J. (Wah.) *Handbook of Pragmatics Highlights*. Amsterdam: John Benjamins Publishing Company. kur. 50-70. https://doi.org/10.1075/hoph.8.04wod.

Zhai, Y., Lu, Y. na Wu, Q. (2023) "Patriotism, Nationalism, and Evaluations of the Government's Handling of the Coronavirus Crisis". *Frontiers in Psychology* 14:1016435. https://doi.org/10.3389/fpsyg.2023.1016435.